ISO 9001:2015 Certified

The Regulator

Linatolewa bure

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISSN: 0856 - 8030 TOLEO NAMBA 3/2025 JULAI - SEPTEMBA 2025 TOLEO MAALUM

Utangazaji kipindi cha Uchaguzi

Kanuni zasisitiza uwajibikaji, maslahi ya Taifa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Taasisi yenye viwango vya ISO 9001: 2015

Kampeni ya SITAPELIKI

Baadhi ya malengo ya kimkakati kwenye Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano yenye ufanisi, ya uhakika na imara na matumizi yake kuendelezwa.

Vilevile ni kuhakikisha kuwa utendaji na ufanisi huduma zinazosimamiwa na ulinzi wa wadau vinaendelezwa na kuimarishwa.

TCRA na watoa huduma za mawasiliano wanaendesha kampeni ya elimu kuhusu namna ya kujilinda dhidi ya ulaghai mitandaoni. Kaulimbiu ya kampeni hiyo ni "SITAPELIKI" na malengo yake ni:

- **i.** Kutoa mwongozo wa usalama mtandaoni na namna watumiaji na wananchi wanavyotakiwa kujilinda dhidi ya ulaghai.
- **ii.** Kuhimizwa watumiaji na wananchi kuripoti matukio ya ulaghai kwa vyombo husika.
- **iii.** Kuwakumbusha watumiaji kutumia njia rasmi za kupata huduma.

Ujumbe wa kampeni

1. Linda taarifa zako kwa kutumia nywila (neno siri) thabiti na tofauti kwa kila akaunti.
2. Usifuate maelekezo na kushirikisha nywila (neno siri) au namba ya uthibitisho (OTP) yako na mtu yeyote.
3. Linda taarifa zako kwa kuepuka kubofya viunganishi usivyovifahamu kwenye barua pepe unazopokea. Ukipata changamoto piga namba 100 ili uhudumiwe.
4. Hakiki namba zako za simu ya mkononi kupitia *106#. Aidha usipokee maelekezo yoyote kwa namba usiyoifahamu.
5. Usiruhusu utapeli wa simu au SMS unaofanyika kimtandao. Ripoti utapeli kwenye namba 15040.
6. Usitekeleze maelekezo yoyote kutoka kwa mtu anayejitambulisha kuwa mtoa huduma ikiwa amekupigia kutoka namba isiyokuwa 100. Mtoa huduma wako wa mtandao wa simu atawasiliana nawe kwa namba 100 pekee. Kuwa makini.
7. Ukipata changamoto katika huduma ikiwemo matumizi ya data, muda wa maongezi, jumbe fupi, piga namba 100 ili uhudumiwe au fika kwenye duka la mtandao husika lililo karibu nawe.
8. Elewa namna kifurushi chako cha data kinavyotumika. Bofya *147*00# ili kudhibiti matumizi ya data bila kifurushi.
9. Kabla ya kufanya malipo au kununua bidhaa mtandaoni, hakikisha tovuti uliyoichagua inatumia itifaki salama ya Mawasiliano (HTTPS). Ikiwa huna uzoefu wa kukamilisha manunuzi mtandaoni tumia huduma ya wakala aliesajiliwa ili kukamilisha manunuzi.
10. Usimpe mtu mwingine taarifa zako binafsi kwenye mtandao kupitia viungo visivyojulikana au baruapepe zisizo na miadi. Wahalifu wanaweza kutumia njia hii ya kufanya utapeli, ikiwemo utapeli wa kifedha.

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 3/2025. Julai-Septemba 2025. Toleo maalum

The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoianzisha TCRA inaipa Mamlaka wajibu katika majukumu yafuatayo:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda maslahi ya watumiaji;
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi;
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu;
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
   (i) Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
   (ii) Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
   (iii) Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

MKAKATI WA TCRA 2021/22-2025/26 NA MALENGO YA KIMKAKATI

Mamlaka imeandaa malengo mbalimbali ili kufikia maono yake katika kukabiliana na mambo muhimu kama yalivyobainishwa katika uchambuzi wa hali halisi ya kisekta. Malengo hayo ni:-

1. Kukuza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta yenye usalama, ufanisi na imara;
2. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya kielektroni na posta zenye ubora na unafuu;
3. Kuimarisha ubunifu wa huduma zinazodhibitiwa, uandaaji wa maudhui ya ndani na ujanibishaji;
4. Kuimarisha ufanisi wa huduma zinazodhibitiwa na kuwalinda wadau; na
5. Kuimarisha uwezo wa taasisi.

MATOKEO YA MKAKATI

1. Kupatikana kwa huduma za mawasiliano za uhakika na salama;
2. Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu;
3. Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
4. Kukua kwa ufanisi wa sekta ya mawasiliano na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo, kanuni ndogo na viwango kwa wadau wa sekta ya mawasiliano; na
5. Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.

SERA YA UBORA

Kutokana na nguvu za kisheria za kusimamia sekta za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta Tanzania, TCRA imejizatiti kuweka mazingira mazuri kwa wenye leseni kwa kutoa rasilimali, kudumisha na kuendelea kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ubora ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora na nafuu kwa watumiaji ili kukidhi matakwa ya Sheria na ya kiudhibiti.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Mhandisi. Mwesigwa Felician

Katibu
Bw. Rolf Kibaja

Wajumbe
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

Mhariri Uzalishaji
Bw. Isaac Mruma

Anwani ya ofisi za uhariri
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz;
dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu

12 Mapya kwenye kanuni za utangazaji



05 Wajibu wa vyombo vya utangazaji kipindi cha uchaguzi

14 Usimamizi unaondeleza ujumuishi

08 Misingi ya taaluma ya utangazaji wa maudhui

22 Tanzania yavuka malengo intaneti



BARUA YA MHARIRI

Weledi, uwajibikaji kufanikisha utangazaji wa uchaguzi

Watanzania waliojiandikisha kupiga kura wataenda vituoni tarehe 29 Oktoba mwaka huu kumchagua Rais, Wabunge na Madiwani. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni mmojawapo wa wadau wakuu wa uchaguzi huu.

TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za mawasiliano ambao watafanikisha shughuli za uchaguzi kwa namna mbalimbali. Watoa huduma watawezesha watu kuwasiliana kwa ufanisi, kutuma na kupokea pesa na kufanya miamala kupitia simu zao na kutumia mitandao ya intaneti.

Vilevile watawezesha Watanzania kuangalia televisheni, kusikiliza redio, kutumia mitandao ya kijamii na kutuma na kupokea barua, vifurushi na vipeto kwa usalama na ufanisi.

TCRA inasimamia huduma za maudhui ya utangazaji, Inafuatilia uzingatiaji wa kanuni na miongozo mbalimbali.

Kanuni hizi ni pamoja na zile maudhui ya utangazaji vipindi vya uchaguzi wa vyama vya siasa.

Kanuni zinazosimamia maudhui, bila kujali iwapo zimetokana na mafunzo waliyopata wanahabari au zinatokana na kanuni zilizotungwa kwa mujibu wa sheria, zinaweka misingi ya uripoti wa shughuli za uchaguzi.

Wakati wa uchaguzi, vyombo vya utangazaji vinapaswa kuwajibika kwa hali ya juu zaidi. Vina majukumu ya kutoa elimu kwa wapiga kura, kufahamisha umma mwenendo wa kampeni za vyama, na kuripoti hali halisi siku ya kupiga kura na matokeo yanapotangazwa.

Kanuni zinalenga kuviwezesha vyombo vya utangazaji kuweka mizania ya matangazo, na kutokubagua kundi lolote katika jamii wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha haviegemei upande wowote. Pia zinataka vyombo vya utangazaji kuhamasisha weledi na maadili ya utangazaji.

Makala na nyaraka kwenye toleo hili zimetokana na rejea zifuatazo:

1. Taasisi ya Media Institute of Southern Africa (MISA) tawi la Tanzania. Imechapishwa kwenye https://tanzania.misa.org/issues-we-address/media-and-elections-issues/
2. Baraza la Habari Kenya (Media Council of Kenya). Wajibu wa vyombo vya habari kuzuia uvunjifu wa amani kwenye michakato ya Uchaguzi (The role of the media in preventing violent electoral processes) Imetolewa https://mediacouncil.or.ke/media-center/mck-media/corporate-blog/role-media-preventing-violent-electoral-processes
3. Shirika la Umoja wa Mataifa ya Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). https://www.unesco.org/en/freedom-expression-rule-law/media-elections.
4. Profesa Tawana Kupe. Wajibu wa vyombo vya habari katika uchaguzi. Uchambuzi wa kina (The Role of the Media in Elections: A Critical Reflection). Imetolewa www.elections.org.za
5. Pili Mtambalike. Wajibu wa vyombo vya habari kwenye kuripoti uchaguzu. Mada iliyotolewa kwenye mojawapo ya semina za mafunzo ya uandishi. Imechapishwa www.engage.or.tz
6. Dr. Abdallah Katunzi, Mada kwenye mkutano wa Wadau wa waandishi kuhusu uchaguzi, Julai 2025.
7. Mhandisi Andrew Kisaka wa TCRA. Wasilisho kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa utangazaji, Dodoma, Februari 2025.
8. Tovuti ya TCRA- https://www.tcra.go.tz/documents/regulations.

UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU

Maudhui bora kwa ustawi wa Watanzania

Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

Mojawapo ya majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni kusimamia huduma za maudhui ya utangazaji kwa Tanzania Bara.

Mpango Mkakati wa TCRA, unaoendelezwa kila wakati, unataja hatua za kuwezesha kuwepo huduma za utangazaji zilizo imara na thabiti Tanzania.

Masuala muhimu kwenye Mkakati huo ni pamoja na kuchangia katika kujenga jamii inayowezeshwa na huduma za mawasiliano.

Maudhui bora ya utangazaji yanachangia ustawi wa Watanzania kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kusambaza taarifa sahihi na kutoa maudhui yenye tija kuhusu shughuli za uchumi kunawezesha wawekezaji wa ngazi mbalimbali kufuatilia fursa na hivyo kuchangia kwenye kujenga uchumi.

Maudhui kuhusu ujasiriamali na matangazo ya biashara kupitia vyombo vya utangazaji wigo wa watumiaji wa huduma na bidhaa. Yanachangia kukua kwa ajira na uchumi kwa ujumla.

Maudhui yenye elimu yanaongeza na kupanua uelewa wa wasikilizaji, watazamaji na wasomaji kwenye mambo mbalimbali.

Hii inarahisisha utoaji huduma kwa watu wanaoelewa, na ambao wanaweza kujenga hoja za kuboresha shughuli za uendeshaji na utawala.

Watoa huduma wanatakiwa kuepuka maudhui yenye mwelekeo wa taharuki na hofu. Elimu na uelewa wa jamii kwenye masuala mbalimbali vinajenga mshikamano wa kitaifa. Kwa ujumla wake vyote hivi vinaimarisha taifa.

TCRA imetoa leseni kwa watoa maudhui ya redio na televisheni za kawaida, za mitandaoni na blogu.

Hawa ni wadau muhimu kwenye mchakato wote wa uchaguzi. Wanatakiwa kuzingatia kanuni na miongozo ya jumla ya utoaji na mahsusi kwenye maudhui kipindi cha uchaguzi.

Wajibu wa vyombo vya utangazaji kipindi cha uchaguzi

Na Mwandishi wetu

Majukumu ya vyombo vya utangazaji kwenye kuripoti uchaguzi yanatokana na misingi sita mahsusi kwa utoaji maudhui yanayochangia maendeleo ya demokrasia.

Vyombo hivi vinatakiwa kuhabarisha, kufanya uchambuzi, kuelimisha, kuwa mlinzi, kutoa jukwaa la midahalo na mijadala na kuwakilisha jamii.

Maana ya kipindi cha uchaguzi kinachosimamiwa na kanuni ni pana. Ingawaje michakato ya vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi inaanza mapema, vyombo vya habari vinatakiwa wakati wote kuzingatia kanuni za uandishi.

Kanuni zinawabana kipindi cha uteuzi, yaani Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inapowatangaza wagombea katika nafasi mbalimbali, kwenye kampeni, siku ya kupiga kura, na matokeo yanapotangazwa.

Vyombo vya utangazaji ni vyanzo muhimu vya taarifa za wagombea, vyama na ilani zao. Pia vinafanya kazi kama mlinzi wa kanuni zilizowekwa na Tume na vyombo vingine ambavyo ni wadau wakuu wa mchakato wa uchaguzi.

Uripoti wa vyombo hivi unawezesha watu kujua iwapo chama, wagombea au taasisi yoyote wanafuata misingi ya uchaguzi huru na wa haki.

Vinatakiwa kutoa majukwaa kwa vyama na wagombea kutangaza sera na ilani zao.

Vinatakiwa kutoa taarifa zitakazowafanya wapiga kura kufikia uamuzi kwa kuelewa wagombea, vyama vyao, sera na ahadi kwenye ilani husika.

Kwa kuripoti kwa uwazi, vyombo hivi vinawezesha mchakato wa uchaguzi kuonekana kuwa ni wazi na unaoeleweka.

Ili viweze kutekeleza majukumu haya, ni lazima vyombo vya utangazaji vizingatie maadili ya uandishi, kanuni na miongozo ya utoaji wa maudhui ya utangazaji kipindi cha uchaguzi.

Kanuni zote za uandishi zinatumika kipindi hiki. Kanuni mahsusi za utangazaji wa maudhui zinaweka msisitizo kwenye maeneo yanayolenga moja kwa moja masuala ya kuendeleza demokrasia.

MAKALA KUU

Umuhimu na upekee wa huduma za utangazaji

Na Mwandishi wetu

Watoa huduma za maudhui ya utangazaji wana majukumu makubwa kwenye kuchangia na kuhamasisha maendeleo ya jamii kwa njia mbalimbali.

Umakini mkubwa zaidi utahitajika kipindi cha kati ya Agosti na Novemba mwaka huu wakati Tanzania ikiwa kwenye hatua mbalimbali za uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Utangazaji na uendeshaji wa vyombo vinavyotoa huduma za maudhui ni shughuli ambazo mlengo wake hutegemea umma.

Habari sahihi zinazoelimisha, kuburudisha, na kuhabarisha zinapaswa kutolewa kwa umma bila kuvuruga mfumo wa maisha au kuleta taharuki au kuumiza watu.

Televisheni na redio zinasambaza mawimbi ya sauti au picha kwa hadhira pana kupitia njia za kielektroniki za mawasiliano ya umma.

Zinatumia mchanganyiko wa viwezesho vya matamshi au aina nyingine za sauti, data, maandishi, picha au michoro ikijumuisha vikaragosi na vitu vingine vinavyoendana na hivyo; iwe mnato au jongefu.

Vyombo hivi vinafikia walengwa kwa namna vyombo vingine haviwezi. Utangazaji unafikia watu wengi, hata wasiojua kuandika na kusoma na bila malipo. Hii ni faida mojawapo ya utangazaji ukilinganisha na vyombo vingine.

Maudhui yanawafikia na kusikilizwa au kutazamwa na watu ambao sio lazima wawe wateja wa mtoa huduma.

Maudhui ya utangazaji ni yale yanayotolewa na vyombo vya mawasiliano vinavyolenga jamii na vinavyotumia masafa, namba, misimbo au mifumo ya mawasiliano

Muda wa rejea ya maudhui yanayotolewa na redio na televisheni ni mfupi; yaani maudhui yakishatoka yanaweza kufikia watu wengi hata kama yataondolewa au kusahihishwa. Utangazaji unahusisha maudhui ambayo yanaathiri watu kwa namna tofauti.

Utangazaji ni njia pekee ya mawasiliano inayowafikia watu wengi kwa haraka na wakati huo huo. Maudhui yanawafikia na kusikilizwa au kutazamwa na watu ambao sio lazima wawe wateja wa mtoa huduma, yaani hata wasiolipia huduma.

Vilevile muda wa rejea ya maudhui yanayotolewa na redio na televisheni ni mfupi; yaani maudhui yakishatoka yanaweza kufikia watu wengi hata kama yataondolewa au kusahihishwa.

Utangazaji unawezesha kuenezwa kwa bidhaa mbalimbali kwa umma moja kwa moja au kupitia matangazo ya watu wengine. Kwa namna ulivyo, utangazaji unafikia jamii kwa ujumla bila kujali iwapo wanaofikiwa wamejiunga na huduma inayotolewa.

Matangazo ya redio na televisheni yanasikika na kuonekana miongoni mwa jamii nzima na kwa wakati uleule. Kwa hali hii ya kuhudumia jamii na umma, utangazaji unapaswa kuweka maanani matarajio ya watu wa aina tofauti na hisia zao. Unatakiwa uridhishe wadau wote.

Maadili ya taaluma

Maadili ya kitaaluma ni misingi na viwango vya maadili vinavyotawala tabia na mwenendo wa watu binafsi ndani ya taaluma fulani. Inaangazia majukumu na matarajio ya wataalamu kwa wateja wao, wafanyakazi wenzao, waajiri, na jamii kwa ujumla.

Maadili ya kitaaluma husaidia kuhakikisha uadilifu, uaminifu na uwajibikaji ndani ya taaluma husika, na hivyo kuchangia katika uaminifu na sifa yake.

Maadili ya utangazaji ni jumla ya misingi, kanuni na viwango vinavyoongoza utendaji kazi wa wahusika kwenye sekta hii. Wahusika hawa ni wenye vituo vya utangazaji, yaani wenye leseni za TCRA na waandishi, watangazaji na wote wanaohusika kwenye kuandaa na kutoa maudhui.

Lengo la maadili ni kuhakikisha wahusika wanafanya kazi kwa kuwajibika, kwa kuzingatia misingi ya kazi zao na kufuata sheria.

Ufanisi wa utangazaji unapatikana pale wahusika wanapotoa maudhui kwa namna yanavyozingatia maslahi ya umma, kujenga imani ya wateja wao na kuzingatia sheria na kanuni.

Yote haya yanapatikana kwa kuzingatia kanuni, ambazo zinaongoza utoaji wa maudhui. Maadili yanaendeleza uandishi unaowajibika kwa jamii na kwa wateja wa vituo.

Vitu vikubwa vya kuzingatia ni usawa, usahihi na uandishi unaozingatia maadili. Kanuni mojawapo inayohakikisha uzingatiaji maadili ni uhuru wa waandishi, yaani wawe huru kuandika na kutangaza bila vishawishi na kutokuyumbishwa.

Wadau na uzingatiaji maadili

Uzingatiaji maadili ya utangazaji ni muhimu kwa wadau wote. Weledi unawezesha serikali kukidhi matarajio ya kujenga jamii yenye uelewa, inayoimarisha utamaduni na yenye amani na utulivu.

Watoa huduma watapata wateja zaidi wa maudhui yao na wanaotangaza biashara na huduma kwenye vyombo vyao, zaidi kwa kuwa na weledi. Watangazaji mmoja mmoja na kwa ujumla wao wataheshimika zaidi kwa kuonyesha weledi.

Watumiaji wa huduma za utangazaji- wasikilizaji redio, watazamaji televisheni, wasomaji wa maudhui ya blogu wataridhika na kinachotolewa. Watangazaji wa biashara watafikia watu wengi

ambao wanajiunga na vituo vyenye weledi na kutembelea akaunti mitandaoni zinazokidhi mahitaji yao ya ubora. Jamii itaondokana na kero na kadhia na maudhui yasiyofaa.

Misingi ya taaluma ya utangazaji wa maudhui

Na Mwandishi wetu

Taaluma ya utangazaji na utoaji wa maudhui kwa umma inaongozwa na misingi inayosisitiza ukweli, kutokupendelea upande wowote na uwajibikaji.

Ukweli

Ukweli ni jambo au kitu kinachoweza kuthibitishwa kwa vigezo vinavyokubalika. Utangazaji una wajibu wa kuutafuta ukweli na kuuripoti kwa ukamilifu.

Vyombo vya maudhui vinatakiwa kufanya kila jitihada kutafuta taarifa zote. Kwenye uandishi kuna kanuni ya msingi inayosema ukiwa na mashaka, tafuta mpaka upate ukweli. Ikiwa bado una mashaka, acha kuitoa taarifa husika. Unaweza kuendelea kuifuatilia taarifa hiyo na kuitoa kwa kuzingatia kanuni.

Uhuru wa kutoegemea upande wowote

Utangazaji unatakiwa kutofuata au kufungamana na upande wowote, na kutohusika na upande wowote unaoweza kuwa na mgogoro wa kimaslahi. Unatakiwa kuwa sawa kwa wadau wote.

Usawa

Pamoja na kuwa huru na kutofungamana na upande wowote, utangazaji na uandishi wa Habari hutakiwa kuonyesha kutoegemea upande wowote na kuweka mizania katika utangazaji wake. Mizania pia inahusu aina ya maudhui yanayotolewa na kituo, na hadhira. Kituo kiwezeshe wadau na jamii kwa ujumla na shughuli zao kuwa kwenye maudhui.

Kuzingatia madhara ya kutangaza jambo

Si kila jambo linaloweza kutangazwa linatakiwa kutangazwa. Iwapo kiwango cha madhara ni kikubwa katika jamii si vema kutangaza. Ni vyema wanahabari wanaoripoti uchaguzi na masuala ya kisiasa kuelewa kwamba kunakuweko mihemuko na hisia miongoni mwa wagombea na vyama vyao.

Haya yasipo ripotiwa kwa weledi yanaweza kuleta hali ya sintofahamu na pia kuchochea vurugu.

Uwajibikaji

Chombo cha utangazaji au mtangazaji anatakiwa kuwajibika iwapo kuna jambo amelitangaza pasi na kuzingatia maadili ya utangazaji au taaluma ya utangazaji.

Uwajibikaji ni pamoja na kutambua makosa ya kiuandishi na uripoti kwa ujumla na kuyarekebisha au kuomba radhi kwa mujibu wa kanuni.

Kuepuka Udhalilishaji na kukashifu

Hili ni suala la kisheria lakini pia ni la kimaadili kwa wanahabari. Waandishi hawatakiwi kutangaza masuala ambayo yana ua sifa ya mtu. Vyombo vya utangazaji vinatakiwa kuepuka maudhui yanayodhalilisha watu au yanayowabagua kwa namna yoyote.

Uthibitishaji wa chanzo cha maudhui

Utangazaji na Taaluma ya Habari inaelekeza juu ya umuhimu wa kutambua chanzo cha Habari. Tatizo hili linajitokeza kwenye uripoti wa vyombo vya habari mitandaoni.

Vingi vinatumia vyanzo vya habari vya upili, yaani kutumia taarifa zinazotolewa na watu wengine bila kuzithibitisha au kupata ufafanuzi na maelezo au nyongeza rasmi kutoka kwa wahusika.

Usimamizi wa maudhui

Na Mwandishi wetu

Usimamizi wa huduma za utangazaji Tanzania, unafanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Umuhimu wa kusimamia maudhui unatokana na upekee wa redio na televisheni kama njia ya mawasiliano kwa umma.

Kwa ujumla wake usimamizi wa sekta unalenga kuweka mfumo na masharti ya utoaji huduma na kuvifuatilia kupitia kanuni na miongozo.

Usimamizi unahakikisha kwamba raslimali za taifa zinazotumika kwenye huduma, kama vile masafa ya utangazaji na mawasiliano yanayotumika kwa ufanisi na kwa manufaa ya taifa.

Masafa ya utangazaji ni pamoja na yanayowezesha huduma za maudhui ya redio na televisheni.

Utangazaji unawezesha kuwepo demokrasia kwa maana ya sauti za watu wa aina mbalimbali kusikika, na kulinda misingi ya demokrasia na utawala bora. Usimamizi unalenga kuhakikisha maudhui vipindi vya uchaguzi yanaendeleza murua wa kitaifa.

Usimamizi unazuia watu kupata madhara kupitia matamshi, maandishi au picha zinazojenga chuki, kuendeleza uhalifu. Vilevile unahakikisha ubora wa maudhui na utoaji maudhui kwa kuzingatia misingi ya ukweli na usahihi. Unathibiti utoaji wa matangazo yanayopotosha.

Usimamizi unawezesha kuweka mizania ya mahitaji ya wadau wa utangazaji kwenye maudhui yanayotolewa. Wadau hao ni pamoja na serikali, jamii kwa ujumla na wasikilizaji wa redio, watazamaji wa televisheni na wasomaji wa maudhui kwenye blogu mitandaoni.

Usimamizi unahakikisha maudhui yanalinda utu wa watu, lakini pia yanazuia unyanyapaa wa makundi ya watu. Utangazaji unawezesha wasikilizaji na watazamaji kuelewa mifumo ya utawala na demokrasia na nafasi zake kwenye uchaguzi.

Sababu za usimamizi wa maudhui zinatokana na mambo ambayo yanakusudiwa kuwezeshwa na usimamizi huu. Kwa upana, masuala hayo ni:

1. Ujenzi wa jamii inayoheshimu misingi ya sheria.
2. Kuongeza uelewa wa Watanzania katika masuala mbalimbali.
3. Kuendeleza tunu za utamaduni halisi wa Watanzania.
4. Kujenga jamii yenye unyoofu
5. Kujenga misingi imara kwa watoto kwa maslahi ya Taifa.
6. Kuepusha watoto na vijana kuiga mambo yasiyo na asili ya Tanzania.
7. Kuendeleza lugha ya Kiswahili.
8. Kuendeleza ajenda za kitaifa.
9. Kujenga mshikamano wa kitaifa na maelewano.
10. Kuendeleza demokrasia.
11. Kuchangia ujenzi wa Taifa kwenye maeneo mengi.
12. Kuendeleza matumizi bora na sahihi ya mtandao wa intaneti.
13. Kuimarisha amani na usalama wa nchi.
14. Kuendeleza maudhui ya ndani, ya Kitanzania na ya jamii.
15. Kuwezesha watu kufanya shughuli zao bila kubughudhiwa.
16. Kulinda jamii dhidi ya maudhui yanayoweza kuwaumiza.
17. Kuhakikisha watumiaji wanapata huduma bora.
18. Kuendeleza taaluma ya uanahabari.
19. Kujenga imani ya watu kwa vyombo vya habari.
20. Kuunga mkono usimamizi.

MATUKIO

Kanuni za maudhui ya redio, televisheni

Na Mwandishi wetu

Kanuni za maudhui ya redio na televisheni zimefanyiwa marekebisho mara kwa mara. Kwa ujumla, zina sehemu yenye matakwa/masharti ya utoaji huduma. Masharti ya jumla yanataja mambo yafuatayo:

Matakwa ya jumla kuhusiana na vipindi

Mwenye leseni/mtoa huduma atahakikisha kuwa vipindi na utoaji wake:

a. Vitazingatia mamlaka ya kitaifa, umoja wa taifa, maslahi ya taifa, ulinzi wa taifa na maslahi ya kiuchumi ya Tanzania.

b. Vinatoa picha ya tunu za kiutamaduni za Kitanzania na utambulisho wake.

c. Vinazingatia staha na heshima.

d. Vinaimarisha uadilifu miongoni mwa umma.

e. Vinaepuka kuingilia faragha binafsi za watu.

f. Haviharibu sifa za watu binafsi.

g. Vinaepuka matangazo ya ubashiri wa kishirikina, ushirikina, tiba za waganga wa jadi.

h. Vinaepuka vipindi vinavyohusiana na utoaji wa maudhui yanayohusiana na ubashiri wa kishirikina, ushirikina na tiba za waganga wa jadi wanaojifanya wanaweza kutibu maradhi.

i. Vinaepuka kubagua na kudhalilisha watu kwa misingi ya jinsia.

j. Havichochei au kuendeleza chuki au kukashifu kundi lolote la watu kwa misingi ya mbari, rangi, dini, jinsia, ugonjwa au ulemavu.

k. Kutokutangaza jambo ambalo lina matumizi ya lugha chafu, maneno ya kufuru au kumtukana Mungu au Imani za watu.

l. Kuwasilisha masuala ya kujamiiana kwa undani na namna ya kuudhi na kuchukiza.

Uwasilishaji habari

Mtoa huduma atahakikisha kwamba kituo kinatenga muda kila siku kwa ajili ya habari. Habari zinatakiwa kuwa sahihi, zisiegemee upande wowote na pia zisiwe na ushabiki. Vilevile zizingatie mizania bila kuhama kutoka kwenye ukweli kwa makusudi, bahati mbaya, kuongeza chumvi au kuacha baadhi ya taarifa na hivyo kufikisha ujumbe usiokusudiwa.

Watoa huduma wahakikishe kwamba ufadhili wa kipindi hauathiri usahihi na mizania kwenye maudhui ya kipindi husika.

Maoni na Utoaji maoni binafsi

Pale ambapo mtoa huduma ameruhusu utoaji wa maoni binafsi wakati wa kipindi, wasikilizaji au watazamaji wataelezwa mapema na kupewa fursa ya kujibu hoja zinazotolewa.

Mtoa huduma ahakikishe kwamba maoni, yawe yametolewa na mtoa huduma mwenyewe au mtu aliyealikwa kutoa maoni yanaonyesha kuzingatia ukweli na yanawasilishwa sawasawa na kwa uwazi, kwa manufaa ya umma.

Makatazo

Wenye vituo wasitoe vipindi vinavyotoa maelezo kuhusu njia za kujinyonga/kujiua, kutengeneza baruti/milipuko au matumizi ya madawa ya kulevya.

Wasitoe muda mrefu isivyo kawaida wakati wa taarifa za habari, au matukio au burudani kwa wamiliki wa vituo kujitangaza.

Wasitoe vipindi ambavyo vitachochea machafuko ya kijamii na miongoni mwa umma.

Wasitangaze vipindi vinavyochochea ukahaba na matendo mengine yasiyo na staha.

Wawe na maudhui kwa watu wenye changamoto mbalimbali. Hizi ni pamoja na za kusikia, kuona, kusimama au kukaa.

Kuzingatia haki na utu

Mwenye leseni apime athari za maudhui kwa haki na utu wa watu wenye ulemavu, wa viungo au matatizo ya

akili

Wenye leseni wasitangaze vipindi vinavyochochea nongwa/unyanyapaa dhidi ya watu wenye changamoto

Wanapotoa vipindi vyenye kuhusisha matumizi ya nguvu wahakikishe kwamba matukio hayo hayahusishwi na watu wenye matatizo ya akili.

Mahojiano

(2) Mwenye leseni ataonyesha kujali wanapotangaza mahojiano na watu waliofiwa, wahanga wa matukio

Waathirika wa ukatili kijinsia, ubakaji

Mtoa huduma hatatoa utambulisho wa mhanga wa matendo ya kiovu au ukatili wa kijinsia isipokua tu pale ambapo mhanga ataridhia kuwa atambulishwe; na akubali kwa maandishi.

Utambulisho wa watoto wahanga wa ubakaji au ukatili na uhalifu mwingine hauruhusiwi

Watoa huduma waepuke kurudia rudia undani wa matukio ya ukatili au uhalifu wa kijinsia.

Mahojiano na mtu mwenye matatizo ya akili

- Mahojiano yasiwe ya kumdhalilisha au kudhalilisha watu wake wa karibu
- Kuwe na mtu wake wa karibu
- Dawa za kutibu zisioneshwe au kutajwa

Lugha

Kanuni kuhusu lugha zinasisitiza kuhusu:

1. Watoa huduma kuhakikisha kuwa Kiingereza na Kiswahili tu vinatumika kwenye vipindi. Kanuni zinakataza kuchanganya lugha.
2. Lugha iwe sanifu. Waepuke kutumia lafudhi zinazopoteza maana ya maneno. Hii ni pamoja na kuwa makini kwenye matumizi ya herufi 'L" na 'R' kwenye matamshi.
3. Kuepuka kutumia lugha isiyo sahihi.
4. Lugha isiyo kamili. Mfano ni kukatiza maneno.
5. Kuweka alama za vituo pasipostahili.
6. Kutokutumia lugha inayolenga kupotosha au kuleta taharuki na hali ya kukata tamaa.
7. Kuepuka kufuru za kidini na kuzingatia hisia kali za kiimani ya kiutamaduni na kidini na kiimani.
8. Kuepuka matumizi ya lugha yenye matusi kwenye vipindi.

Matangazo mubashara

Mtoa huduma anayeamua kutoa matangazo mubashara atatakiwa kuwa na uwezo wa kiufundi wa kuweza kutoa matangazo mubashara ili kuepuka kutoa maoni kwa lugha chafu na isiyokubalika kutoka kwa watangazaji, washiriki wa kipindi, na wanaopiga simu. Uwezo wa kiufundi ni pamoja na kuwa na vifaa vya kuchelewesha sauti kwenda hewani kwa sekunde kadhaa na kuizuia isitoke iwapo ina utata.

Kuepuka Ubaguzi

Mtoa huduma atatakiwa:

- Kuepuka kutangaza vipindi ambavyo vinachochea na kupamba ubaguzi kwa misingi ya asili ya mtu, rangi, utaifa, mbari, uasili, jinsia, umri/rika au mahitaji maalum.
- Kuonesha wanaume na wanawake kama watu walio na uwezo sawa kwenye kuhimili masuala ya jamii.
- Kuepuka kuwaelezea watu kama kundi badala ya watu kama mkusanyiko wa watu mbalimbali.



Mapya kwenye kanuni za utangazaji wa redio na televisheni

Na Mwandishi wetu

Tunawasilisha maeneo muhimu kwenye marekebisho ya Kanuni za Utangazaji wa Redio na Televisheni Tanzania ambayo yalifanyika mwaka 2024. Marekebisho hayo yaliongeza vipengele kadhaa kwenye kanuni na pia kwenye tafsiri na maelezo ya maneno yaliyotumika. Kanuni hizo zimechapishwa kwenye touvti ya TCRA, kiungo https://www.tcra.go.tz/documents/regulations.

Jina

Kanuni hizi zinajulikana kama Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) (Marekebisho) za mwaka 2024 na zinasomwa pamoja na Kanuni za mwaka 2018 ambazo humu zitaitwa "Kanuni Kuu".

Marekebisho ya Kanuni ya 3

Kanuni kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri na maelezo ya maana ya maneno kama ifuatavyo:

"Vitendo vya kujamiiana/ngono" ni vitendo vyovyote vinavyofanywa kwa kugusa sehemu za siri za mtu mwingine, au kutoa ishara zinazoashiria kujamiiana/ ngono, ama kwa kutumia ishara zinazomaanisha kujamiiana/ngono au kutumia vidude vya ngono au kuonekana kutenda jambo lolote linalohusisaha matiti, uchi wa mwanamke na wa mwanaume; ikiwa ni pamoja na kufanya vitendo vya kujamiiana au vitendo vingine ambavyo vinaweza kusababisha mhusika au wahusika kujamiiana/kufanya ngono.

"Maudhui ya kujamiiana/ngono" ina maana ya maudhui yaliyo na vitendo vya kujamiiana/ngono.

Marekebisho ya Kanuni ya 8

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 8 kwa kuongeza mara tu baada ya kipengele cha 2 cha kanuni hii kipengele kipya kinachosomeka:

"(3) Mwenye haki ya kufikisha mawimbi ya utangazaji nchini hatabeba chaneli za utangazaji zenye maudhui ya ndani ya Tanzania ambayo hayakutolewa/kusambazwa chini ya leseni iliyotolewa na Mamlaka."

Marekebisho ya Kanuni ya 14

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 14 kwa kufuta maelezo yaliyoko pembeni na badala yake kuweka haya yafuatayo:

"Vipindi vinavyotazamwa au kusikilizwa na watu kwenye familia"

Nyongeza ya Kanuni 14A

Kanuni Kuu inarekebishwa kwa kuongeza mara tu baada ya kanuni ya 14 kipengele kipya (kuhusu muda wa vipindi vinavyofaa watu wazima tu):

14A.-(1) Mwenye leseni ya huduma za maudhui anaweza kutoa vipindi vinavyofaa watu wazima muda wa vipindi vinavyofaa watu wazima.

(2) Pamoja na kipengele cha (1), uwasilishaji wa vipindi unatakiwa kuzingatia tunu, mila na utamaduni wa taifa.

(Maelezo ya Mhariri: "Muda wa vipindi vinavyofaa watu wazima ni kuanzia saa sita usiku hadi saa 11 alfajiri. Watoa huduma wanatakiwa kutoa vipindi vinavyofaa watu wazima tu muda huu. " Vipindi vya familia kutazama televisheni au kusikiliza redio" ni vile ambavyo vinafaa kwa familia yote wakiwemo watoto na vinavyoweza kutolewa nje ya muda wa vipindi vinavyofaa watu wazima tu."

Marekebisho ya Kanuni ya 17

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kukata na kuondoa kanuni ya 17 na badala yake kuweka maneno yafuatayo (kuhusu utoaji wa maoni binafsi):

17.-(1) Mwendesha kipindi/mtangazaji hataruhusiwa kutoa maoni binafsi wakati wa kipindi.

(2) Pamoja na kipengele cha (1), mwenye leseni anaweza kumruhusu mgeni au mchambuzi ambaye ana sifa za kuzungumzia mada inayojadiliwa kutoa maoni yake binafsi, na wasikilizaji au watazamaji wapewe taarifa mapema na kuchangia mada na maoni yanayotolewa."

Nyongeza ya Kanuni 17A

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara moja baada ya kanuni ya 17 kanuni mpya (kuhusu kuzingatia umakini mkubwa):

17A.-(1) Mtoa huduma za maudhui hatatangaza vipindi ambavyo:-

a. Vinatoa maelezo ya njia za kujiua, kutengeneza milipuko na matumizi ya madawa ya kulevya.

b. Vinatoa nafasi kwa muda mrefu kuliko kawaida kwa wamilki wa vyombo na vituo vya utangazaji kwenye habari na taarifa za matukio, vipindi vinavyoelezea masuala au vinavyoburudisha.

c. Vinaweza kuchochea machafuko.

d. Vinaweza kuchochea umalaya na shughuli nyingine za uasherati."

(2) Pamoja na kipengele cha (1), mtoa huduma za maudhui atachukua tahadhari kubwa anaporipoti matukio ya watu kuteswa, watu au wanyama kufanyiwa mambo mabaya, picha zinazoonesha kwa karibu maiti au miili iliyokatika, watu walioko kwenye maumivu makali au kwenye hatua za kifo au watoto wanaofanyiwa ukatili.

Marekebisho ya Kanuni ya 19

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 19(k) kwa kufuta maneno "zingatia" yanayotokea kati ya maneno "hadhira" na "kwa" na kuweka badala yake maneno "kama ilivyoelezwa."

Marekebisho ya Kanuni ya 22

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 22(3) kwa kufuta maneno "matukio" yanayoonekana kati ya maneno "na", na "hakikisha", na badala yake kuweka maneno "matukio mubashara yenye maslahi ya taifa."

Nyongeza ya Kanuni ya 26A

Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara moja baada ya kanuni ya 26 kanuni mpya ifuatayo (kuhusu idhini ya kusoma maudhui ya gazeti, kitabu au makala):

26A.-(1) Mtoa huduma za maudhui hatasoma maudhui ya magazeti, vitabu na makala wakati wa kuwasilisha kipindi bila kuwa na idhini ya maandishi ya mmilki wa vitu hivyo.

(2) Pamoja na kipengele (1), mtoa huduma za maudhui anayekusudia kusoma magazeti, vitabu au makala wakati wa kuwasilisha vipindi vyake atasoma tu vichwa vya habari na si vinginevyo."

Marekebisho ya Kanuni ya 28

Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 28 na badala yake kuweka ifuatayo (kuhusu uzingatiaji wa tunu, mila na utamaduni wa taifa):

28.-(1) Mtoa huduma za maudhui ataweka maanani uzingatiaji wa tunu, mila na utamaduni wa taifa wakati anapotoa vipindi vinavyohusisha na vyenye maudhui ya kujamiiana/ngono.

(2) Bila kuzingatia kipengele cha (1), mtoa huduma za maudhui hatafanya yafuatayo:-

(a) Hatatoa maudhui ya kujamiiana/ngono.

(b) Hatarusha matangazo kutoka vyanzo vingine au kuruhusu kupitishwa kwenye chombo chake maudhui yoyote yanayoonesha au kuhusisha vitendo vya wazi vya kujamiiana/ngono.

(c) Hatatangaza na kuonesha sehemu za vipindi zenye picha au maelezo ya viungo vya uzazi.

3) Pale mtoa huduma anapotangaza vipindi vinavyohusisha maudhui ya kujamiiana/ngono, atafanya hivyo kwa namna ambayo inazingatia tunu, mila na utamaduni wa taifa.

Marekebisho ya Kanuni ya 33

Kanuni kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 33 kwa kufuta kipengele cha 3.

Marekebisho ya Kanuni ya 38

Kanuni kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 38 kwa:
(a) Kufuta aya (c) inayoonekana kwenye kipengele (7).
(b) Kuweka namba mpya kwenye aya (d) na (e) ziwe (c) na (d) mtawalia.

Marekebisho ya Kanuni ya 39

Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 39 kwa kufuta kipengele za (1) na badala yake kuweka:

"(1) Mtoa huduma za maudhui atachapisha ratiba ya vipindi na mpangillio wake kwenye chaneli yake au majukwaa ya mtandaoni angalau siku 14 kabla ya kuanza kutumika."

Usimamizi unaoendeleza ujumuishi

Na Mwandishi wetu

Moja ya malengo ya kimkakati ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta zinazotolewa nchini Tanzania zinapatikana na ni nafuu kwa wote.

Hatua za kiusimamizi kwenye sekta hii zimewezesha kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu na utoaji wa huduma katika maeneo yasiyofikika kirahisi na yasiyo na huduma za kutosha. Watoa huduma hawaendi maeneo haya kutokana na sababu za kibiashara.

Hatua hizi pia zimechochea kupungua kwa gharama za huduma (bei na tozo nafuu za huduma na kuimarisha imani ya watumiaji wa mitandao. Vilevile, zimechangia kuongeza upatikanaji wa vifaa bora vya mawasiliano na vyenye viwango. Pia zimeimarisha ufahamu/ uelewa wa watumiaji.

Uelewa huo unahusisha kampeni za elimu kwa umma kuhusu matumizi bora ya huduma na tahadhari dhidi ya udanganyifu/ulaghai wa kimtandao.

Kuongezeka kwa uelewa na imani ya watumiaji katika huduma kumesaidia kuongeza matumizi na upanuzi wa huduma.

TCRA imefanikiwa kushughulikia kwa ufanisi vipengele muhimu vinavyochochea ushirikishwaji. Hivyo ni:

- Miundombinu imara,
- Teknolojia inayopatikana na yenye bei nafuu (vifaa na ushuru),
- Uelewa wa watumiaji,
- na Ujuzi wa kidijitali.

Jukumu la TCRA katika kukuza ushirikishwaji linahusisha kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora, nafuu, na zinazopatikana kwa urahisi. TCRA hutekeleza kanuni, sheria na masharti ya leseni ili kuhakikisha jukumu hili linafanikiwa.

Kanuni hizi zinafafanua mahitaji muhimu.

Leseni zinazotolewa na TCRA zinakuwa na masharti ya leseni yanayokuza msingi wa upangaji mzuri wa mitandao na upanuzi wa huduma.

Mfano wa hivi karibuni wa masharti kwenye leseni ni leseni zilizotolewa kwa matumizi ya masafa kwenye vitalu vinne wa wizo wa masafa wa megahezi (Mhz) 3600-3800.

Watoa huduma wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanaweka miundombinu na kuwa na mitandao katika makao makuu yote ya mikoa kiutawala katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo mwaka 2033.

Vilevile huduma zao zinapaswa kufikia angalau mikoa sita (6) tofauti ifikapo mwaka 2028.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Bakari, anasema kuwa usambazaji wa mitandao na huduma kwa kutumia masafa haya unatarajiwa kuendeleza miundombinu na uwezo wa huduma za mitandao ya kasi.

Hatua hiyo itapanua utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu kwa idadi kubwa ya watanzania na kuchochea maendeleo ya uchumi wa taifa, hususan uchumi wa kidijitali, pamoja na kurahisisha ukuaji wa sekta nyingine.

Kanuni za ushuru zinahitaji bei za huduma ziwe zenye uhalisia, haki na zinazozingatia gharama halisi.

Vilevile, kanuni zinazohamasisha watoa huduma kuchangia uwekaji wa miundombini ili kupunguza gharama zimeharakisha kasi ya kueneza huduma sehemu nyingi Tanzania.

Kanuni za Ubora wa Huduma zinaweka viwango vya ubora kwa huduma mbalimbali, zikiwa na lengo la kujenga imani ya watumiaji katika huduma hizo.

Unafuu wa gharama za matumizi umewapa watumiaji nchini Tanzania chaguo pana zaidi la teknolojia na huduma kati ya mwaka 2021 na mwaka huu.

Takwimu za sekta ya mawasiliano za Septemba 2025 zinaonesha kuwa gharama maongezi kwa simu za mkononi zilipungua mara sita kati ya Septemba 2019 na Septemba 2025.

Gharama za kupiga simu ndani ya mtandao mmoja zilipungua kutoka shilingi 185 hadi 26, huku gharama za kupiga simu kwenda mitandao mingine zikishuka kutoka 192 hadi 29.

Wastani wa gharama za vifurushi ulipungua kwa asilimia 540, kutoka shilingi 37 kwa dakika hadi 5.8, na gharama ya ujumbe mfupi mmoja (SMS) ilipungua kwa asilimia 1,874, kutoka shilingi 168 hadi 8.10.

Mitambo kwenye minara ya simu za mkononi iliongezeka kwa asilimia 12 ndani ya mwaka mmoja tangu Septemba 2024.

Serikali, kupitia Mfuko wa Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote (USCAF), imejenga na kuboresha zaidi ya vituo 1,000 vya mawasiliano katika mikoa yote.

Maboresho haya ya miundombinu yamehusisha kuhamia katika vizazi vipya vya teknolojia ya simu kuanzia uzao wa pili (2G), tatu (3G), nne (4G), hadi tano (5G).Ripoti inaonyesha kuwa mikoa yote nchini sasa ina angalau kituo kimoja chenye teknolojia ya 5G.

Ripoti ya hivi karibuni ya Umoja wa Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO) imeeleza kuwa sera thabiti na mfumo shirikishi wa usimamizi vimechochea maendeleo na kukua sekta ya mawasiliano Tanzania.

Mikakati ya kufikia maeneo ya vijijini nayo imechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji huu. Ushirikishi pia unahusu kuwezesha watu wengi zaidi kupata na kufikiwa, kuchukuwa kwa matumizi na kumudu huduma za mawasiliano.

Januari 2023, TCRA ilichapisha mwongozo wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa watu wenye ulemavu (WWU). Mwongozo huo unawataka watoa huduma za mitandao ya simu kuwa na wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya kuwahudumia na kuwasiliana na watu wenye ulemavu.

Watoa huduma wanatakiwa pia kuonyesha matumizi ya vifaa kwa WWU kwa njia na muundo unaowarahisishia kuelewa na unaofaa.

Vilevile, wanapaswa kutoa matangazo na promosheni za bidhaa na huduma zilizoundwa mahsusi kwa watu wenye ulemavu katika miundo inayoweza kufikiwa na kundi hilo.

Ufuatiliaji wa TCRA kwa watoa huduma za mawasiliano ya simu hivi karibuni umebaini kuwa wengi wanazingatia matakwa haya.

Tanzania yapita malengo intaneti yajizatiti matumizi teknolojia za kisasa

Na Mwandishi wetu

Matumizi ya intaneti Tanzania yamepita lengo la Serikali la kufikisha huduma hiyo kwa asilimia 80 kutokana na kasi ya kusambaza miundombinu inayowezesha matumizi ya teknolojia za kisasa za mawasiliano.

Uchambuzi wa ripoti ya hivi karibuni ya hali ya mawasiliano nchini unaonesha kwamba kasi ya kuchakata data imeongezeka karibu mara tatu ndani ya miaka minne, na simu janja zikienea kwa asilimia 40 ndani ya miaka miwili.

Takwimu za hali ya mawasiliano kati ya Julai na Septemba 2025, zilizotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dr Jabiri Bakari zinaonesha ukuaji wa kasi wa sekta za mawasiliano na utangazaji. Vilevile taarifa inaweka picha ya namna sekta ya posta inavyosuasua.

Tanzania imetekeleza miradi mbalimbali ya kubadili hali ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ndani ya miaka minne iliyopita. Hii ni pamoja na kujenga miundombinu maeneo ya vijijini na yasiyofikika kwa urahisi na kuhimiza na kuwezesha matumizi ya teknolojia za kisasa za mawasiliano.

Kulikuwa na watumiaji wa intaneti **56,322,287** Septemba mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 94 kutoka Machi 2021.

Intaneti ilikuwa imeenea miongoni mwa watu kwa asilimia 49 Machi 2021. Takwimu za Septemba 2025 zinathibitisha kuwa huduma hiyo imeenea asilimia 82.6 kwa watu, pointi 2.6 juu ya lengo ya Serikali la asimilia 80 ifikapo mwisho wa mwaka huu.

Matumizi ya data kwa mwezi yaliongezeka kwa asilimia 167 kati ya Septemba 2023 na Septemba 2025 – kutoka petabaiti 92 hadi petabaiti 246. Ongezeko kutoka Juni 2025 lilikuwa asilimia 17. Petabaiti ni kipimo cha ukubwa wa data kwenye kompyuta na vifaa vya kielektroniki vyenye sifa ya kompyuta.

Asilimia 99.5 ya watumiaji wa intaneti Tanzania wanapata huduma hiyo kupitia vifaa vya mkononi, vikiwemo simu janja, vishkwambi na modemu.

Ripoti inaonesha kuwa vishkwambi vimeemea miongoni mwa watu kwa asilimia 0.67, kutoka 0.80 na modemu kwa asilimia 1.09 kutoka moja (1) kati ya Septemba 2024 na Septemba mwaka huu.

asilimia 290

Kasi ya kupakia data iliongezeka kwa asilimia 290 kati ya Machi 2021 na Septemba 2025, kutoka megabaiti kwa sekunde (MBps) 6.6 hadi 26. Ongezeko lilikuwa asilimia 50 kutoka Juni mwaka huu.

Uwezo wa ndani wa matumizi ya intaneti uliongezeka kwa asilimia 267 kati ya Septemba 2023 na Septemba mwaka huu, kutoka gigabaiti kwa sekunde (Gbps) 1,040 hadi 2,649. Hata hivyo, watumiaji wa Tanzania wanachukua asilimia 15 tu ya kiasi cha uwezo wa intaneti ulioko nchini.

Jumla ya uwezo wa intaneti ni Gbps 17,590 wakati kupakua na kupakia data kunatumia Gbps 2,646 tu, na kuacha Gbps 14,941 kutotumika.

Uzao wa tatu wa teknolojia za mawasiliano ya mkononi (3G) umezidi kuenea kwa pointi asilimia 10.8 zaidi kati ya Septemba 2023 na Septemba mwaka huu. Kuenea uzao wa nne (4G) kumeongezeka kwa pointi 8.9 kipindi hicho.

Kufikia Septemba 2025, uzao wa tatu umeenea miongoni mwa watu kwa asilimia 93.8 kutoka 90 Septemba 2024 na kijiografia kwa asilimia 75.9, kutoka 74.

Uzao wa nne (4G) umenea kwa watu asilimia 94.2 na kijiografia kwa asilimia 76.9 kulinganisha na asilimia 85 na 70 mtawalia kipindi tajwa.

Uzao wa tano (5G), ambao uliingia Tanzania 2022 una kasi, ufanisi na kuaminika zaidi na unawezesha vifaa vingi vya mawasiliano ya kielektroniki kuunganishwa

wakati mmoja na hivyo kushirikisha watumiaji wengi. Ulienea asilimia 28.9 miongoni mwa watu na kijiografia kwa asilimia 8.6 Septemba 2025.

Kuenea kwa uzao huu kijiografia kuliongezeka mara nne, kutoka asilimia 2.2 hadi 8.6 ndani ya mwaka mmoja. Ulienea miongoni mwa watu kwa pointi 10.9 za asilimia- kutoka asilimia 18 hadi 28.9 Septemba mwaka huu.

Ripoti inaeleza kuwa kulikuwa na minara 9,745 ya mawasiliano ya mkononi iliyofungwa vifaa 43,669 vya uzao wa pili (2G), 3G, 4G na 5G.

Mikoa yote ina minara yenye angalau seti moja ya vifaa vya mawasiliano ya mkononi ya 5G. Dar es Salaam, Dodoma, Mjini Magharibi, Mwanza, Arusha na Mbeya inaongoza kwa kuwa na vifaa vingi zaidi vya 5G.

Ripoti inaeleza kuwa laini za 5G ziliongezeka kwa asilimia 18.9 kati ya Juni na Septemba 2025, kutoka 1,312,013 hadi 1,561,208.

Jumla ya laini za simu za mkononi zilizosajiliwa kwa teknolojia zote hadi Septemba zilikuwa 99,184,6321. Kati yake 98,165,650 zinatumika kwa mawasiliano miongoni mwa watu na 1,130,140 kwa mashine.

Teknolojia ya mawasiliano ya mashine kwa mashine, inayojulikana kama M2M kwa kifupisho chake kwa Kiingereza, inawezesha vifaa kuwasiliana vyenyewe kwenye mitandao bila kuhusisha binadamu.

Vifaa hivyo ni pamoja na kamera za kurekodi matukio ambazo zenye laini zinazowezesha kupokea na kutuma data zenyewe kutoka mbali.

Laini za mezani, huduma inayotolewa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) ziliongezeka kwa asilimia 40 kati ya Juni na Septemba 2025 na kwa asilimia 56 kulinganisha na Machi 2021.

Huduma za televisheni kidijitali mfumo wa ardhini (DTT) zinafumiwa na asilimia 58 ya watu. Zimeenea asilimia 33 ya eneo la nchi. Televisheni kwa satelaiti zimefikia watu na kuenea kijiografia kwa asilimia 100.

Mawimbi ya redio ya FM yanatumiwa na asimilia 84 ya watu na yanafika asilimia 59 ya eneo la Tanzania.

Huduma za posta na usafirishaji vifurushi zimekuwa na mwenendo wa kupanda kwa muda mfupi na kushuka. Vitu vilivyopostiwa kwenda nje ya nchi kati ya Juni na Septemba mwaka huu vilipungua kwa asilimia 124 na kwa asilimia 235 kulinganisha na Machi 2021.

Vilivyopokelewa kutoka nje ya nchi vilipungua kwa asilimia 17 na 235 mtawalia kipindi tajwa.

Jipatie nakala yako bure

Jarida hili linakuwezesha kupitia na kupata stadi mpya na pia kupanua mtandao wako wa watu wenye weledi kama wewe. Kupata nakala za bure za jarida hili na kuwasilisha maoni, tuma barua pepe kwa

regulator.magazine@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz

Tunakaribisha maoni na hoja kutoka kwa wasomaji wetu. Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu ya bure kwenye namba ya wateja wa TCRA, ambayo ni **0800008272.**

Soma kujisajili

Jedwali 1: Vidokezi muhimu na uchambuzi wa ripoti ya robo mwaka

Mabadiliko inamaanisha asilimia ya kuongezeka au kupungua

	2025			2021	
Maelezo	**Sept. 2025**	**June 2025**	**Asimilia ya ongezeko kulinganisha na Juni**	**Machi 2021**	**Asilimia ya ongezeko kulinganisha na Machi 2021**
Laini za simu	99,184,621	92,656,179	7	52,813,930	88
Laini za simu mawasiliano ya watu	98,165,650	91,652,443	7	52,813,930	86
Laini za simu mawasiliano ya machine zenyewe	1,190,140	1,083,355	10	Huduma haikuwepo	-
Kuenea laini kwa watu (%)	145.7	136.1	Pointi 9.6	89	Pointi 56.7
Simu za mezani	111,169	79,619	40	71,313	56
Watumiaji waliojiunga na intaneti	56,322,287	54,078,530	4	29,071,817	94
Kuenea intaneti kwa watu (%)	82.6	79.3	3	49	Pointi 33.6
Matumizi ya data (kwa petabaiti)	738	633	17	117	531
Akaunti za pesa kwa simu	71,662,233	68,059,290	5	32,720,180	119
Kuenea simu janja kwa watu (%)	39.5	37	Pointi 2.5	22	Pointi 17.5
Wastani wa gharama za maongezi kwenye vifurushi (shilingi kwa dakika)	5.8	5.4	Imeongezeka kwa asilimia 7	9	Imepungua kwa asilimia 35
Wastani wa gharama za maongezi bila vifurushi (shilingi kwa dakika)	27	27	Hazikubadilika	63	Zimeshuka kwa asilimia 133
Ving'amuzi vya TV vilivyokuwa hewani	2,315,641	2,035,319	-	2,810,663	Kupungua kwa asilimia 21
Huduma za posta na usafirishaji vifurushi					
Vitu vilivyopostiwa nje ya nchi	27,479	61,602	Vimepungua kwa 124%	92,118	Idadi ilipungua kwa 235%
Vitu vilivyopokelewa kutoka nje ya nchi	65,691	76,784	Pungua kwa 17%	219,865	Idadi ilishuka kwa 235 %
Ulinganisho na takwimu za 2023 na 2024	**Jul-Sept 2025**	**Aprili-Juni 2025**		**Jul-Sept 2023**	**Ongezeko kulinga-nisha na Sept. 2023**
Kuenea kwa watu uzao wa tatu (3G) (%)	93.8	93.4	Pointi 0.4	83	10.8
Kuenea uzao wa nne (4G) kwa watu (%)	93.8	92	Pointi 1.8	74	Pointi 19.8
Kuenea kijiografia 3G (%)	75.9	75	Pointi 0.9	67	Pointi 8.9
Kuenea kijiografia 4G (%)	76.8	75	Pointi 1.8	55	Pointi 21.8
Kuenea uzao wa tano (5G) kwa watu (%)	28.9	26	Pointi 2.9	12 (Machi 2024)	Kulinganisha 2024 ni pointi 16.9
Kuenea kijiografia 5G (%)	8.6	5.9	Pointi 3	2.2	Pointi 6.4
Vikoa vya dot tz	35,621	34,342	4%	28,601	Asilimia 24.5%
Wastani wa gharama za maongezi kwenye vifurushi (shilingi kwa dakika)	12,475	13,839	Zimeongezeka kwa asilimia 7	23,328	Imepungua kwa asilimia 28
Ving'amuzi vya TV vilivyokuwa hewani	2,315,641	2,035,319	Kuongezeka kwa 14%	3,052,068	Kupungua kwa asilimia 32
Kuenea utangazaji hadi Septemba 2025					
Kuenea televisheni mfumo wa ardhini (DTT) kwa watu –asilimia 58. Kijiografia asilimia 33					
Kuenea televisheni kwa setilaiti kwa watu na kijiografia – asilimia 100					
Kuenea mawimbi ya redio ya FM kwa watu – asilimia 83.9. Kijiografia – asilimia 59.1					
Chanzo: https://www.tcra.go.tz/services/statistics					

Sekta ya mawasiliano katika namba

Usajili wa laini za simu (P2P na M2M)



7.1% ongezeko kati ya Juni - Sept 2025, ikiashiria mwelekeo chanya katika soko la mawasiliano.

Laini **milioni 98.2** zilitumika katika mawasiliano ya **P2P**	Laini **milioni 1.1** zilitumika katika mawasiliano ya **M2M**

Karibu **theluthi** ya watumiaji wa laini za simu **kupitia P2P** walitumia mtandao wa Vodacom



Wanaume 51.5%

Wanawake 48.5%

Watumiaji wa intaneti wazidi kuongezeka

Milioni 54.1 Juni 2025 ▲ **4.1%** **Milioni 56.3** Septemba 2025

Milioni 26.9 Idadi ya simu janja hadi Septemba 2025 kutoka milioni 25 Juni 2025 huku ueneaji wake ukifikia **39.5%**

Mgawanyiko wa huduma ya intaneti kwa kila mtoa huduma hadi Septemba 2025



Zaidi ya **robo tatu (81.3%)** ya watumiaji wa intaneti Tanzania wanatumia Yas, Vodacom, na Airtel

Mwenendo wa watumiaji wa intaneti



Matumizi ya Pesa Mtandao yazidi kushika kasi Tanzania

Idadi ya akaunti zinazotumia pesa mtandao zaongezeka kwa 5.6%

Juni 2025 **Milioni** **68.1**

5.6%

Septemba 2025 **Milioni** **71.7**

Vodacom inaongoza soko kwa zaidi ya theluthi moja ya jumla ya akaunti za pesa mtandao ikifuatiwa kwa karibu na Yas

Mwenendo wa akaunti za pesa kwa kila mtoa huduma hadi Septemba, 2025

	Machi 2025	Juni 2025	Septemba 2025
Airtel Money	12,077,797	11,722,925	12,940,606
Azam Pesa	38,399	38,212	185,586
Halo Pesa	5,830,634	6,249,543	7,182,997
Mixx by Yas	20,182,931	20,672,815	21,482,792
T- Pesa	1,508,952	1,355,046	518,650
M- Pesa	26,903,563	28,020,749	29,351,702
Jumla	**66,542,276**	**68,059,290**	**71,662,333**

Wanufaika wa huduma ya visimbuzi waongezeka kidogo

14%

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ili kupata huduma za utangazaji za televisheni vimeongezeka kwa **14%** kutoka **milioni 2** hadi **milioni 2.3**

73.6% **DTH** | **26.2%** **DTT**

Azam Media Limited ilikua na visimbuzi **1,645,172** hadi Septemba 2025 ikiwa ni **71%** ya visimbuzi vyote vilivyopo nchini

Televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya



Mwenendo wa visimbuzi kwa kila mtoa huduma kufikia Septemba 2025

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024	Machi 2025	Juni 2025	Septemba 2025
Azam	1,277,763	1,069,703	1,356,664	1,340,135	1,290,048	1,344,752	1,645,172
Continental	68,862	68,862	68,968	67,663	66,697	63,873	62,612
DStv	238,467	233,607	234,415	225,263	234,064	189,272	192,628
Star media Limited	2,120,591	536,311	477,236	477,527	444,238	417,618	397,970
Zuku	25,094	23,106	21,687	21,335	22,098	19,804	17,259

Huduma za kiposta, usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Bidhaa za kiposta

564,846

zilitumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Septemba 2025.



Karibu nusu ya bidhaa hizo za kiposta ni vifurushi

Jumla ya masanduku na mifuko binafsi

158,073

yalitolewa hadi Septemba 2025, kiwango sawa na kilichorekodiwa Julai, 2025

Teknolojia ilivyobadilisha utangazaji

Na Mwandishi wetu

Vyombo vya utangazaji vinatumia teknolojia inayobadilika wakati wote. Teknolojia imepanua nguvu ya vyombo vya utangazaji kufikiwa watu wengi na kwa ufanisi zaidi. Imewezesha kuhama kwa utangazaji kutoka mfumo wa analojia kwenda dijitali.

Vilevile muingiliano wa teknolojia umewezesha huduma za utangazaji kupatikana kwa njia mbalimbali. Hili limepanua wigo wa maudhui kufikia watu wengi zaidi na kwa wakati wanaopendelea.

Maudhui yanapatikana kwenye vifaa vingine vya mawasiliano kama vile simu za mkononi, vishkwambi na kwenye mitandao ya intaneti na mitandao ya kijamii kwa kutumia vifaa hivi na vingine.

Maudhui yaliyorushwa muda wowote na mahali popote yanapatikana kwa urahisi kama mtumiaji anavyotaka. Kutokana na changamoto ya maudhui yaliyorushwa muda usioruhusiwa kwa maudhui ya rika zote kupatikana saa ambazo watu wote wanayapata, kunakuwa na umuhimu wa watumiaji kujisimamia wao wenyewe.

Teknolojia zinatoa fursa za wanahabari kufanya kazi kwa ufanisi. Zimeendeleza utandawazi, kukua mahusiano ya jamii kutokana na yenyewe, biashara, uwekezaji, na upashanaji habari. Kila mwenye simu janja anaweza kuchakata maudhui na kuyasambaza bila kuzingatia kanuni za utangazaji.

TEHAMA imeleta mahusiano ya kiutamaduni kati ya mataifa na changamoto zinazoambatana na muingiliano huo. Imeingiza utamaduni usio wa asili ya Tanzania. Watu wanaiga mitindo, misemo na matamshi yasiyokidhi vigezo vya lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

Baadhi ya vyombo vya habari vinavyojiunga na vya nje ya Tanzania vinatoa maudhui yanayopingana na mila na utamaduni asilia.



Akili Unde

Akili unde ni ujumla wa teknolojia na programu tumizi za kompyuta ambazo zinawezesha mashine na vifaa kufanya kazi ambazo zinafanywa na binadamu. Vilevile zinawezesha kupata maudhui ya masuala mengi kupitia mitandao.

Akili unde inawezesha weledi na kufanikisha shughuli za utangazaji na utoaji maudhui. Mifano ni programu zinazowezesha kuandika, na kuhariri miswada au miongozo ya kuandaa vipindi,

kuhariri makala zinazotoka kwenye blogu na kujibu maswali mengi. Vilevile inawezesha kupata rejea za kutumika kwenye maudhui, kuandaa rasimu ya mawasilisho na hotuba na hata kuandaa taarifa za habari.

Hata hivyo, isipotumiwa vizuri, akili unde itashusha viwango vya uasili kwenye weledi. Itazalisha wanahabari wavivu, wasiojituma na wategemezi kitaaluma.

Wanahabari wanaweza kudidimia kiweledi kwa kuwa wahusika wanatumia zaidi mashine kuliko wao wenyewe kufikiri. Vilevile akili unde inaweza kuchangia makosa ya kikanuni na kusababisha kuendelea ukiukwaji wa maadili.

Akili unde inawezesha kuandaa na kupanga maudhui. Pia yanawezesha watangazaji kufanya rejea ya haraka na kupata picha, video, sauti au nyaraka ya kutumia kwenye taarifa zao.

Akili unde zinaweza kuwa na majibu sahihi lakini bila uhalisia. Iwapo habari wanayoichukua imekosewa basi kosa litaendelea kuwepo. Iwapo maudhui yanayotumiwa ni feki au hayakuzingatia kanuni, au sio taarifa ya awali iliyosahihishwa au kuboreshwa basi ukiukwaji huo utaendelea.

Wanaochukua taarifa kupitia Akili unde wanaweza kutokuzihakiki na kuzipa uhalisia wa jamii wanayofanyia kazi. Matumizi yasiyofaa na kuthibitiwa ya Akili unde kwenye taaluma yanaweza kushusha viwango vya elimu, hivyo vyombo kujikuta vinaajiri watu wakihitimu kwa kudanganya kitaaluma.

Akili unde inaweza kuchochea kuenezwa kwa taarifa na maudhui feki. Video feki zinaweza kutengenezwa kwa kuingiza maneno kwenye wahusika wanaolengwa kutekeleza ulaghai huo kwenye mifumo ya utangazaji.

Kanuni za Maudhui mtandaoni zinakataza matumizi ya akili unde kuandaa na kutoa maudhui ya kutunga na yasiyo na uhalisia.

Umakini unahitajika kwenye kutumia Akili unde kwenye utangazaji. Kuna umuhimu wa kutumia programu zinazoweza kutambua habari feki na kuhakiki vyanzo sahihi vya maudhui.

Hii inaweza kuwa chanzo cha upotoshaji wa vyombo vinavyotumia vyanzo vya upili bila kuthibitisha uhalisia wa taarifa.

Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road,
14414 Dar es Salaam, Tanzania.
Email: dg@tcra.go.tz

@tcra_tanzania